

MARIA NA SIMU ZA CHUPA YA BATI

Maria And The Tin Can Telephone

AUTHOR:
Kate Wanjira Kamau

ILLUSTRATOR:
Bruno Iradukunda



NABU

Dhima ya NABU

NABU ni shirika lisilo la kibiashara lenye makao yake Jijini New York likiwa na namba ya usajili 501(c)(3) na dhima yake ni kutatua tatizo la ukosefu wa uwiano katika utunzi na usambazaji wa vitabu vya watoto, ili kuwasaidia watoto wote kuweza kusoma na kukuza vipawa vyao kamili.

Kuhusu Warsha

Katika mwaka wa 2019 na mwanzo wa 2020, NABU iliandaa semina za waandishi na wachoraji nchini Rwanda ili kuunda vitabu halisi vya watoto kwa lugha ya Kinyarwanda. Warsha ziliundwa ili kuhitimu lengo letu la kushughulikia mahitaji ya vitabu vya watoto katika lugha za mama. Mkurugenzi wa Ubunifu wa NABU, Michael Ross, na Meneja wa Programu za Kenya, Beryl Oywer, wanaendelea na semina hizi katika mkoa mpya wakati Nabu inapojiandaa kuenea katika nchi zingine barani Afrika.

Vipindi hivi vimeundwa ili kupata maoni mapya na mitazamo mpya wa vitabu vya Kiswahili nchini Kenya. Uteuzi wa hadithi za dijitali zilizoundwa katika semina hizi zinajitokeza katika vitabu vilivyochapishwa, na zinapatikana ulimwenguni. Mapato yote kutoka kwa uuzaji wa vitabu vyetu yatasaidia waandishi na wachoraji na mipango yetu ya masomo katika Afrika Mashariki.

NABU's mission

NABU is a New York-based 501(c)(3) non-profit organization, with a mission to solve the imbalance in children's book creation and distribution, so all children can read and rise to their full potential.

About the Workshop

Throughout 2019 and the beginning of 2020, NABU hosted a series of author and Illustrator workshops in Rwanda with the purpose of creating original children's books in Kinyarwanda. The workshops were created as part of our goal to address the need for children's books in mother tongue languages. NABU Creative Director, Michael Ross, and Kenyan Programs Manager, Beryl Oywer, are continuing these workshops in new regions as Nabu expands.

These sessions have been adapted to create fresh ideas and new perspectives for our new Kiswahili collection in Kenya. A selection of the digital stories created in these workshops materialize into printed books, and are available globally. All of the proceeds from the sale of our books will go to support local authors and illustrators and NABU reading programs in East Africa.

NABU & THE AGA KHAN FOUNDATION EAST AFRICA

'Maria and the Tin Can Telephone' is an original NABU title, written by Kate Wanjira Kamau and proudly produced by NABU in collaboration with the Aga Khan Foundation East Africa (AKFEA). AKFEA brings together human, financial and technical resources to address the challenges faced by the poorest and most marginalised communities in the world. Special emphasis is placed on investing in human potential, expanding opportunity and improving the overall quality of life

Hakimiliki © 2019, NABU

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya chapisho hili inayoweza kutolewa tena kwa njia yoyote, kuhifadhiwa katika mfumo wowote, wa kielektroniki, mitambo, nakala, kurekodi, dijitali au vinginevyo - bila idhini ya awali ya mchapishaji.

Copyright © 2019, NABU

All rights reserved. No part of this publication may be reproduced in any form, stored in any retrieval system, or transmitted in any form by any means - electronic, mechanical, photocopy, recording, digital or otherwise - without the prior permission of the publisher.



MARIA NA SIMU ZA CHUPA YA BATI

Maria and the Tin Can Telephone

AUTHOR:
Kate Wanjira Kamau

ILLUSTRATOR:
Bruno Iradukunda

CREATIVE DIRECTOR & EDITOR:
Michael Ross

TRANSLATIONS BY:
Beryl Oywer

Maria ni msichana anayependa michezo mbali mbali, ana nywele ndefu nyeusi na tabasamu nzuri. Maria anaishi mtaa wa Old Town Mombasa na familia na marafiki wake katika eneo mmoja.




Maria is an adventurous little girl, with long black braided hair and a sweet smile. Maria lives in Old Town Mombasa with her family and friends all on one street.

Wakati wazazi wake wamo katika harakati za nyumbani, Maria hutoka nyumbani na kuenda kupatana na marafiki wake wawili wa dhati, Wanjiru na Wanjala na wote kwenda mchezoni.



When her dad and mum are busy around the house, Maria goes out of the house and meets her two best friends, Wanjiru and Wanjala to go on adventures.

Kila mtu katika eneo hilo anajua kwamba marafaiki hawa watatu wanapenda kucheza sana. Wao huenda kutembea na kucheza kila siku.



Everyone in their neighborhood knows how adventurous these three friends are. They go on adventures every day.

Wazazi wa Maria, Wanjiru na Wanjala hawafurahi wao wakienda mbali na nyumbani lakini bado watoto hao hupuuza maneno ya wazazi wao.

Maria, Wanjiru and Wanjala's parents did not like them going too far from home but they did not always listen.




Jioni moja waliporejea nyumbani, mamake Maria aliwaona na kuwaita. Walijua ya kwamba ilikuwa jambo la muhimu kwa kua mamake Maria alionekana mwenye wasiwasi.



One evening as they came back home, Maria's Mother saw them and called them in. They knew this was important because Maria's mother looked worried.

“Kaeni chini hapo mlangoni,” aliwaambia. Marafiki hao walikaa chini na kungojea. “Hii ni siku ya mwisho nyote mtakuwa pamoja kwa muda mrefu,” Mama Maria alinena. “Kwa hivyo muagane sasa.”

“Please sit down by the door,” she said. The friends sat and waited. “This is the last day you are all going to be together for some time” Marias mother said. “You need to say goodbye to each other.”



“Lakini mbona mama?”
Maria aliuliza kwa sauti ya chini.

“But why Mother?”
Maria asked in a low voice.



“Ugonjwa wa Corona sasa umeenea hadi Mombasa na maafisa wa afya wamewaambia watu wote wakaenyumbani ili waepuke kuugua.” Maria, Wanjiru na Wanjala wakaangaliana wakiwa wamechanganyikiwa mno.

“The Corona Virus is now in Mombasa and the health officers have told everyone to stay home to avoid getting sick.” Maria, Wanjiru and Wanjala looked at each other very confused.




“Colola?” Wanjala akauliza. “Hapana si Colola, Corona,” Mamake Maria akasema. “Ni nini hiyo?” Wanjiru akauliza.




“Colola?” Wanjala asked. “No not Colola, Corona.” Maria’s Mother said. “What is that?” Wanjiru asked curiously.

“Ni virusi vinavyoathiri mwili wa mwanadamu hasa mapafu, na kufanya iwe vigumu kupumua. Wengi wa wanaoambukizwa huhisi kama kwamba wanaugua mafua na wengine huzidiwa na hufa”.

“It is a virus that affects the body, especially the lungs making it hard to breath. Many people who get infected feel like they have the flu, but some do die”.




“Kwa hivyo, ili kuepuka maambukizi, sote hatuna budi kubaki nyumbani, kunawa mikono mara kwa mara, kuzingatia usafi na kuvaa barakoa ikiwa ni lazima utoke kwa nyumba,” alielezea polepole.




“To protect ourselves and others we must all stay home, wash our hands regularly, practice good hygiene and wear a face mask if you have to leave the house.” She explained.

Mambo yalikuwa tofauti. Marafiki hao hawangeweza tena kuenda katika ziara zao. Kila mmoja alikuwa nyumbani na barabarani hakuna aliyeonekana.



Things were different. The three friends could no longer go out on their adventures, everyone was home, and the streets were quiet and empty.

Maria, Wanjiru na Wanjala aghalabu walitumia rununu za wazazi wao kupigiana simu lakini walipewa dakika tano kila siku.



Maria, Wanjiru and Wanjala would often use their parent's mobile phones to call each other but could only talk for five minutes a day.

Muda huo bado haukua unatosha. Marafiki hao walihuzunika kwa kuwa mambo yalikuwa tofauti. Iliwabidi watafute suluhisho.



The time was too short. The friends were sad that things were not the same. They had to come up with a solution.

Maria alikumbuka walichosoma shuleni kuhusu simu za kutengenezwa na chupa ya bati na kamba. Jambo hili lilimfurahisha mno.




Maria remembered what they had learnt in school about tin can telephones. This made her very excited.

Alizunguka nyumba akitafuta chupa za bati zilizokuwa tupu na kamba. Mamake Maria na Maria walilizifunga chupa hizo zote pamoja. Walipo maliza, Maria alienda kuacha chupa hizo za bati nje ya nyumba ya Wanjiru na chupa ingine nje ya nyumba ya Wanjala.



She went around the house and looked for empty cans and string. With the help of her mother, they tied them all together. Maria went and dropped one can outside Wanjiru's house and one outside Wanjala's house.

Sasa wanguweza kuzungumza mchana kutwa.
“HABARI RI RI RI...HABARI RI RI RI..HABARI RI RI RI” ndivyo walivyoanza mazungumzo yao kila mara.




They could now talk all day long. . “HABARI RI RI RI...HABARI RI RI RI ...HABARI RI RI RI,” is how they would start every call.

“Msiwe na wasiwasi wenzangu,” Wanjala alinena, “Uwele huu wa corona utaangamizwa hivi karibuni na tutaweza kucheza pamoja tena. Tuwaskize wazazi wetu na tukae ndani ya nyumba na karibuni tutaenda ufuoni kuogelea na kucheza mchana kutwa.”




“Don’t worry my friends,” Wanjala said, “Coronavirus will soon end and we will be able to go on adventures again and play with each other again. We need to listen to our parents and stay inside, but soon we will go outside and go to the beach and swim and play all day.”

Wangetumia ile simu mchana kutwa na usiku kucha. Walikua na furaha sana kwa kuwa hawakuhitaji pesa yoyote kuzungumza, na wazazi wao hawakua na hofu kuhusu usalama wao. “Kumbuka kunawa mikono na kuzingatia usalama.” Hivyo ndivyo walivyoambiana.




They would use the tin can telephones all day and night. They were really happy about it as they did not need any money to talk and their parents did not have to worry about their safety. “Remember to wash your hands and stay safe” they would tell each other.

Maria, Wanjiru na Wanjala waliwaambia marafiki wao wote juu ya simu hii.



Maria, Wanjiru and Wanjala told their friends about the tin can telephone.

Kwa muda sio mrefu, watoto kutoka maeneo ya juu ya Kericho hadi jangwa la Turkana, kutoka juu ya Aberdares na mwambao wa Ziwa Victoria, watoto waliunganishwa kwa njia ya simu hio ya bati. Walifurahi sana mwishowe waliweza kuongea tena.



Soon children from the beautiful highlands of Kericho to the deserts of Turkana, to the top of the Aberdares and the shores of Lake Victoria, children were connected through tin can telephones. They were so happy they could finally talk to each other again.

NABU

Kuhusu Hadithi Za NABU

NABU hutunga hadithi za watoto zenye maudhui ya kitamaduni. Watoto ambao hukumbana na tamaduni na lugha mbali mbali wana uwezo mkubwa wa kutaka kujifunza mengi maishani na kuwa raia wenye huruma kwa wote duniani.

Tunaamini kwamba hadithi zenye maudhui ya kitamaduni zinanzojenga picha ambazo watoto huona wanapojitazama kwenye kioo husaidia watoto kujithamini na kujivunia, na watoto ambao hujifunza tamaduni tofauti na zao wana uwezo mkubwa wa kukuwa watu wazima wanaothamini utu wa maisha ya binadamu na kuboresha ulimwengu kwa faida ya wote.

About NABU Stories

NABU creates children's stories with a cultural point of view. Children who are exposed to multiple cultures and languages are more likely to become lifelong learners and compassionate global citizens. We believe that culturally relevant stories that reflect who children see when they look in the mirror help to develop healthy self-esteem and a sense of pride, and children who learn about cultures different from their own are much more likely to develop into adults who value the dignity of human life and making the world a better place for all.

This series of NABU stories are bilingual, written in both Kiswahili and English, making them ideal for exposing young children to new cultures or helping children of the diaspora connect to the culture of their families.



BRUNO IRADUKUNDA

e. iradubru@gmail.com
m. + 250 783 241 528

Bruno IRADUKUNDA is an artist practicing in the fields of painting, illustration, sculpture and graphic design, and he has been illustrating children's books since 2015. In 2018, the International Board on Books for Young People (IBBY) awarded Iradukunda as one of the best illustrators of the year for his illustrations in "La Troisième Perle", written by Kai HIRWA and published by EDITIONS Bakame. In 2019, Iradukunda was awarded with a certificate from World Bank Group for participating in "reading ready" in Rwanda. Bruno has recently established his own art studio in Rwanda.

MARIA NA SIMU ZA CHUPA YA BATI

Maria and the Tin Can Telephone

NABU



AGA KHAN FOUNDATION

An agency of the Aga Khan Development Network

Canada 

The LEGO Foundation 

nabu.org

110 East 25th Street,
New York, NY 10010